

SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA**05/03/2018****TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Wananchi wote mnatangaziwa kwamba, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania litaondosha kwa njia ya mnada wa hadhara gari chakavu lilipo katika Mkoa wa Dar es Salaam katika ghala lake lilipo eneo la Mikocheni kwa tarehe kama ilivyooneshwa kwenye jedwali.

TAREHE	ENEO/MAHALI MNADA UTAKAPOFANYIKA	MALI ITAKAYOUZWA
20/03/2018	Ghala lililopo Kiwanja Namba. 4, Nyumba za TPDC Mikocheni, Barabara ya Rose Garden/Mikocheni	TOYOTA LAND CRUISER, HARD TOP

VIGEZO NA MASHARTI YA MNADA

1. Chombo/Kifaa kitauzwa kama kilivyo, mahali kilipo;
2. Mnunuzi atalazimika kulipa papo hapo amana (deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya chombo alichonunua, na atatakiwa kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa chombo husika na amana iliyolipwa haitarudishwa;
3. Gharama za kubadilisha umiliki ni jukumu la mnunuzi, mnunuzi atatakiwa kukamilisha umiliki wa chombo alichonunua ndani ya miezi mitatu.
4. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua chombo alichonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo;
5. Ruhusa ya kuangalia chombo husika itatolewa kwa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya mnada; kuanzia saa nne kamili asubuhi hadi saa kumi kamili;
6. Mnada utaanza saa nne kamili (04:00) asubuhi, siku ya Jumanne tarehe 20 Machi, 2018;
7. Vigezo na Masharti ya mnada kuzingatiwa.
8. Wananchi wote mnakaribishwa kishiriki katika mnada huu.

IMETOLEWA NA KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI**SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA****S. L. P 2774****SIMU NA: +255 22 2200103/4, 2200112****NUKUSHI: +255-22-2200113****DAR ES SALAAM****BARUA PEPE: tpdcmd@tpdc.co.tz**